



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Babati itauza mali chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara tarehe **08/06/2024** siku ya Jumamosi.

Mali chakavu zitakazouzwa ni kama zilivyoorodheshwa katika jedwali hapa chini:-

NA	AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA	IDADI
1	Lorry Tipper Isuzu SM 2541	1
2	Kasiki ya kuhifadhi fedha	1
3	Kabineti za chuma	2
4	Pikipiki za magurudumu mawili SM 6936 na SM 5595	2

Masharti ya mnada:-

1. Chombo kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa hapo hapo amana (Deposit) isiyopungua Asilimia Ishirini na T.ano (25%) ya thamani ya chombo/kifaa alichonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo/kifaa husika na amana aliyolipia haitarudishwa.
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa au kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
4. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika.
5. Mnada utanza saa nne (4:00) asubuhi katika Ofisi za Halmashauri ya zamani na karakana ya ujenzi ya Halmashauri – Mrara.

Anna P. Mbogo
MKURUGENZI MTENDAJI (W)